HOTUBA YA MHE. ANGELLAH JASMINE KAIRUKI (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA) KWENYE SHEREHE YA MAHAFALI YA 26 YA CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA TANZANIA, KAMPASI YA TABORA, TAREHE 31 MACHI, 2017

Mheshimiwa Queen Mlozi, Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Tabora;
Dkt. Gunini Kamba, Kaimu katibu tawala wa Mkoa wa Tabora;
Mheshimiwa Leopord Ulaya, Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora;
Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa na Wilaya;
Dkt. Henry Mambo, Mtendaji Mkuu na Mkuu wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania;
Viongozi wa Taasisi na Mashirika ya Umma;
Viongozi wa Dini na Vyama vya Siasa;
Wakurugenzi wa Matawi na Watumishi wa Chuo cha Utumishi wa Umma;
Wahitimu wa Kozi Mbalimbali;
Wageni Waalikwa;
Wanahabari;
Mabibi na Mabwana; Habari za Asubuhi;

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema, aliyetuwezesha kukutana hapa leo tukiwa na afya njema. Aidha, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika Mahafali haya ya 26 ya Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania

Mkuu wa Chuo, Wageni Waalikwa; *Pili,* kabla sijaendelea na hotuba yangu ningependa kuchukua nafasi hii, kuwapongeza wenyeji wetu; Mheshimiwa Kaimu Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ya Tabora kwa mapokezi mliyotupatia, na kukubali kujumuika nasi katika hafla hii. Napenda pia kuwapongeza Viongozi na watendaji wa Kampasi hii, pia kwa mapokezi mazuri, na kwa maandalizi ya hafla hii ya kutunuku vyeti kwa wahitimu wa kozi mbalimbali. Najua wapo waliojitolea muda na nguvu zao kuhakikisha kuwa shughuli hii inafana. Hongereni sana maana tunaambiwa siku zote kwamba ‘ukiona vinaelea, ujue vimeundwa’.

Tatu, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa wahitimu wote ambao leo hii mnatunukiwa vyeti kwa kuhitimu mafunzo yenu. Najua kuhitimu kwenu kumekuja baada ya kuonesha juhudi kubwa na hatimaye kufaulu masomo yenu. Pia nisiwasahau waelekezi wenu pamoja na Watumishi wote wa Chuo ambao kwa umoja wao na umahiri mkubwa waliwezesha mazingira ya kujifunza kwenu ambayo matokeo yake yanaonekana leo. ***Hongereni Sana!***

Mkuu wa Chuo, wageni waalikwa, mabibi na mabwana*;* tunaposherekea mahafali haya, ni muhimu tukajielekeza na kutafakari mazingira tuliyonayo kwa sasa. Mazingira ya dunia ya sasa, na hata yale ya Nchi yetu, yana fursa na pia changamoto zake. Ni ukweli usiopingika kwamba dunia nzima sasa hivi inashuhudia awamu nyingine ya mapinduzi ya kiuchumi na kijamii, ambapo baada ya mapinduzi ya viwanda (Industrial Revolution) yaliyodumu kwa takribani karne mbili zilizopita, katika karne ya 21, dunia inapita katika mapinduzi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Tofauti ya mapinduzi haya, ni aina ya viwanda vilivyopo, na teknolojia inayotumika kuviendesha viwanda, na aina ya rasilimaliwatu inayotumia teknolojia hii. Jambo la msingi ni kwamba, viwanda vimeendelea kuwa nguzo muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Na hii ndiyo fursa kubwa ambayo wahitimu wetu wakiitumia vizuri, itakuwa na manufaa si kwa Taifa letu, bali pia kwao binafsi.

Ndugu Wageni waalikwa, mabibi na mabwana, pamoja na fursa zinazopatikana kutokana na mapinduzi ya teknolojia, hatuwezi kupuuza changamoto zinazotokana na kukuwa kwa teknolojia ya habari na mawasiliano. Kama tunavyofahamu, teknolojia ina kawaida ya kurahisisha kazi, na kupunguza matumizi ya nguvu za binadamu. Athari ya hatua hii ni kuwa kazi ya kufanywa na watu kumi, inaweza kutekelezwa na mtu mmoja; na kwa wenzetu waliokwisha fika mbali wanatumia ‘***robots’*** badala ya binadamu. Mapinduzi haya hayakwepeki kwa kuwa Tanzania ni sehemu ya dunia, na ni muhimu kwetu sote tujipange kutumia fursa zinazotokana na mapinduzi haya, na pia kujiandaa kukabiliana na changamoto zake.

Ndugu wageni waalikwa, napenda niseme kwamba maudhui ya hotuba yangu kwa siku ya leo, ni kuwahamasisha kutumia fursa zinazopatikana kutokana na mwelekeo wa Serikali yetu ya Awamu ya Tano ambayo imedhamiria kujenga uchumi wa viwanda kama njia ya kutuwezesha kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; na kuifanya Nchi yetu kuwa na hadhi ya ‘Uchumi wa Kati’. Ujumbe huu unaihusu Menejimenti ya Chuo, Wahitimu wanaotunukiwa vyeti leo, na wale

wanaoendelea na masomo; na naomba nifafanue kidogo.

Ndugu Wageni waalikwa, historia ya Chuo cha Utumishi wa Umma ni ya muda mrefu, na nisingependa kuirudia kwa kuwa naamini walio wengi, hususan Watumishi wa Umma mnaifahamu. Hata hivyo, napenda kusisitiza kuwa lengo la kuanzisha Chuo hiki ilikuwa ni kuiwezesha Serikali kuwa na wataalamu wa kutosha ili iweze kutimiza malengo yake ya kiutawala, na kuwaletea Wananchi maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Kutokana na kupanuka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii, Chuo hiki kimeendelea kukua kutoka Kampasi mbili zilizokuwepo Miaka ya 1960 hadi 1980, na kufikia Kampasi 6 hivi sasa. Kama alivyoeleza Mtendaji Mkuu, Chuo kina mpango wa kujenga Kampasi nyingine katika maeneo mbalimbali ya Nchi. Kupanuka huku kunaenda sambamba na kubuni na kutoa kozi zaidi ya zile za miaka ya nyuma, ikiwemo Elimu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, na kozi zote hutolewa kwa viwango tofauti hadi kufikia ngazi ya Stashahada. Kukua kwa Chuo hiki, ni ishara tosha kwamba mabadiliko hayakwepeki.

Swali la kujiuliza ni Je, elimu inayotolewa na Chuo chetu itawavusha wahitimu wake kutumia fursa zilizopo na kukabiliana na changamoto zake? Japokuwa hatuwezi kuwa na majibu ya moja kwa moja, zipo dalili za kuelekea huko kutokana na hatua zilizochukuliwa na Serikali kukiwezesha Chuo kutimiza malengo yake ya muda mfupi na mrefu.

Wageni waalikwa, hatua ya kwanza ilikuwa ni kuhakikisha kuwa Chuo chetu cha Utumishi wa Umma kinatoa kozi ambazo zinatambulika katika mfumo wetu wa kielimu ili wahitimu wetu waweze kukubalika katika soko la ajira, badala ya Serikali peke yake. Hatua hii ilihusisha kuandaa mitaala inayokubalika kitaifa. Kutokana na hatua iliyofikiwa napenda kutoa pongezi kwa jitihada za Uongozi wa Chuo zilizopelekea maboresho ya mitaala ya Chuo kwa mujibu wa vigezo vya Baraza la Ithibati la Elimu ya Ufundi (NACTE) na hatimaye kuwawezesha Chuo kupata usajili. Mafanikio haya ni ya kujivunia. Hivyo napenda kuwahakikishia wahitimu mlioko hapa kwamba, vyeti mtakavyovipata leo, vinatambulika katika soko la ajira na pia vinakidhi vigezo vya kujiunga na vyuo vya elimu ya juu kwa ngazi za Stashahada na Shahada ndani na nje ya Nchi. Ni jukumu lenu kuvitumia katika fursa nilizozitaja hapo awali, na pia kuwawezesha kukabiliana na changamoto zake.

Kwa wale mtakaopata ajira Serikalini, tunawatarajia kuwa mstari wa mbele katika suala zima la utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015, sekta binafsi au kujiajiri, wito wangu ni ule ule. Tumieni ujuzi wenu kuchapa kazi kwa kuwa naamini mnayo maarifa ya kutosha.

Kwa wale ambao bado mnaendelea na masomo, jitahidini kwa kuwa Menejimenti ya Chuo inaendelea na jitihada za kuboresha mazingira ya kujifunzia. Napenda kuwaasa mtambue kwamba Kampasi yenu inayo mazingira bora ikilinganishwa na Kampasi nyingine. Hatua kadhaa zimechukuliwa na Menejimenti kuboresha miundombinu ya Chuo kwa kutumia vyanzo vya mapato vya ndani kama vile ujenzi wa jengo la ghorofa mbili katika Kampasi hii ambalo litakuwa na Maktaba, Maabara ya kompyuta na madarasa. Wakati naipongeza menejimenti ya Chuo kwa hatua hii, napenda kuwaasa wanafunzi na wanajamii wengine katika Chuo kulitunza maana ndio mnaolitumia kila siku. Likitunzwa vizuri litawasaidia hata watoto wenu au hata Watanzania wengine.

Mtendaji Mkuu wa Chuo, wageni waalikwa mabibi na mabwana, Pamoja na hatua ya kuboresha miundombinu, ninazo taarifa kuwa Chuo kimekamilisha Rasimu ya mafunzo mapya yatakayokuwa ya lazima kwa kila Mtumishi wa Umma kwa lengo la kuboresha Utumishi wa Umma. Aidha, nimearifiwa kuwa Chuo kimechukua hatua za kuanzisha Shahada ya Kwanza ya Uhazili pamoja na ile ya Menejimenti ya Kumbukumbu na Nyaraka. Ni dhahiri kuwa hatua hizi zinaonesha kukua kwa Chuo na kubadilika kuendana na mahitaji ya soko. Ninawaahidi ushirikiano wangu wa dhati katika kuyafanikisha haya yote na Ofisi yangu iko wazi kwa ushauri na Mwongozo pale utakapohitajika ili sote kwa pamoja tufanikishe adhma hii njema mapema iwezekanavyo.

Kwenu Wahitimu; Ni matumaini yangu kwamba leo kila mmoja wenu ni mwenye furaha. Hivyo basi, nitumie nafasi hii tena kuwapongeza Wahitimu wote kwa kuifikia siku hii ya kihistoria katika maisha yenu. Natambua kuwa baadhi yenu ni Watumishi wa Umma na wengine mtajiunga kwenye Utumishi wa Umma baada ya muda si mrefu.

Napenda kutoa rai kwenu kuwa, mafunzo mliyopata hapa chuoni yasiishie kuwa na vyeti vya kuhitimu tu, bali yawe ni nyenzo ya kufanya kazi kwa kasi mpya yenye ufanisi ili kuleta tija kwa ajili ya kukuza na kuendeleza uchumi wa Taifa letu. Ninawasihi kuwa, huu usiwe mwisho wa kujiendeleza kwani mafunzo huongeza ujuzi, weledi na mbinu za ufanisi wa kazi hususani katika

kujifunza teknolojia mpya. Waajiri pote nchini wanaelewa umahiri wa wahitimu toka Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) katika utendaji bora wa kazi. Hivyo, nawaasa kuwa Mabalozi wa Chuo na muelewe ninyi ni kiungo muhimu katika utendaji kazi wa siku hadi siku. Nawaagiza mkawe waadilifu na wachapakazi mtakapokuwa katika majukumu yenu ili kulinda imani ya Chuo kwa wadau mbalimbali.

Ndugu Wahitimu*;* Natambua kuwa leo sio siku ya hotuba ndefu, lakini nitumie nafasi hii tena kuendelea kuwasihi kwamba, sasa ni wakati wenu wa kuonesha tofauti kati ya aliyemaliza Chuo cha Utumishi wa Umma na ambaye hajapitia Chuoni hapa.

Na hili litadhihirika tu kwa kufanya kazi kwa weledi mkubwa wenye kuzingatia Kanuni, Sheria na Taratibu za Utumishi wa Umma katika kutekeleza majukumu kwa ufanisi kwa kuonesha uwezo wa kumudu majukumu **(Competence),** uadilifu **(Integrity)** na kutoa huduma bora kwa Wananchi na sio kufanya kazi kwa mazoea **(business as usual)** ili kuendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya Tano inayosisitiza uwajibikaji na uadilifu kwa kauli mbiu ya ***“Hapa Kazi Tu”.***

Nikiwa Waziri mwenye dhamana nya Utumishi wa Umma nawahakikishia kuwa Serikali yenu itaendelea kutengeneza fursa za ajira katika Utumishi wa Umma kadri uwezo wa Serikali kiuchumi utakavyoruhusu.

Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana*;* Napenda kutumia fursa hii pia kuwaagiza Waajiri wote na Watumishi wa Umma kwa ujumla wao kuweka mkazo katika kuwapatia Watumishi mafunzo ya awali ndani ya miezi sita.

Aidha, ni vyema Waajiri wakaona umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya mafunzo ya awali na mafunzo mengineyo ili kuendeleza Watumishi wao kwa mujibu wa mipango ya mafunzo ya taasisi husika. Ili kufanikisha mafunzo haya yote, nawaagiza waajiri kukitumia Chuo hiki kwa mafunzo mbalimbali yanayolenga kuboresha fani na taaluma zilizopo katika sehemu za kazi.

Kwa nafasi yangu kama Waziri mwenye dhamana ya Utumishi wa Umma na kwa kushirikiana na Viongozi wenzangu kwa pamoja tunaahidi kukipa Chuo ushirikiano wa dhati ili kukijengea uwezo zaidi na kukiongezea ufanisi katika utoaji wa huduma ya Taaluma bora na ujuzi katika maeneo yetu ya kazi.

Nimejionea mazingira ya chu na nimesikia changamoto zenu; uchakvu wa miundombinu ya madarasa, mabweni na maabara za kompyuta, tutazifanyia kazi ili kuboresha miundombinu ya

kujifunzia na kufundishia.

Wahitimu na wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana; Kabla sijamalizia hotuba yangu, naomba kutolea ufafanuzi jambo moja ambalo baadhi ya vyombo vya habari ama kwa makusudi au kwa bahati mbaya vimelipotosha.

Nilipokuwa Mbeya, tarehe 22 Machi, 2017 nilizungumzia juu ya mipango ya siku za baadaye ya Wizara yangu kwa kushirikiana na Chuo chetu cha Utumishi wa Umma katika kuandaa mafunzo kwa kada mbalimbali kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Nilisema kwamba, Watumishi wa Umma watakaofikiriwa kuteuliwa katika nafasi za Uongozi/Madaraka itawalazimu wawe wamehudhuria na kufaulu mafunzo hayo. Hata hivyo, baadhi ya vyombo vya habari vikaeneza uvumi kwamba Watumishi wa Umma wote hawatapandishwa vyeo mpaka wasome na kufaulu mitihani ya Chuo cha Utumishi wa Umma.

Huo ni upotoshaji. Mpango wetu wa mafunzo ya lazima na mitihani ni kwa ajili ya Watumishi wa ngazi za uteuzi na siyo Watumishi wote wa Umma. Mpango huu unalenga kuwaandaa na kuwajengea uwezo Viongozi watarajiwa ili waweze kukabiliana vizuri na changamoto za uongozi. Watumishi wengine wataendelea kupandishwa vyeo kulingana na Miundo ya maendeleo ya Utumishi wao.

Wahitimu na wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana; Kwa mara nyingine tena naomba niwatahadharishe kuhusu janga la ***"UKIMWI"*** nyote mnaelewa kuwa elimu na maarifa mliyopata hayatakuwa na maana wala manufaa kwenu binafsi na kwa Taifa kama hamtajihadhari na gonjwa la ***UKIMWI.*** Wengi wenu mpo katika umri wa kutegemewa kama nguvu kazi ya Taifa, Hatuna budi kwa pamoja kuhakikisha kuwa nguvu kazi hii haipotei ila inakuwepo kwa manufaa na maendeleo ya Taifa. Hivyo basi nawaasa kila mmoja wenu achukue hatua za makusudi kujikinga asiambukizwe, na yule aliyeambukizwa basi tumuombe asiambukize wengine ili Taifa letu liwe endelevu kwa kupitia nguvu kazi hii. Siku zote kabla ya kuamua, tukumbuke kujiuliza **tuko wangapiiii?**

Mtendaji Mkuu wa Chuo, Wahitimu, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana; Mwisho, ni imani yangu kwamba ndugu wahitimu wetu mtatumia ujuzi mlioupata kwa maslahi ya Umma. Mkatoe huduma bora kwa weledi na maadili ya hali juu.

Mwisho kabisa, niwaambie Wahitimu Wetu kwamba ninatambua kuwa leo ni siku yenu ya furaha, nisingependa kuwachosha na hotuba ndefu. Nawapongezeni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya hadi kufikia hatua hii. Nawatakieni kila la kheri katika majukumu yenu ya kulijenga Taifa letu.

Mungu Kibariki Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania,
Mungu Ibariki Serikali yetu ya Awamu ya Tano, Mungu Ibariki Tanzania,
Mungu Ibariki Afrika!

Hongereni na Asanteni Sana kwa Kunisikiliza!